

# FORM 3 TERM 3 APRIL 2022

## KISWAHILI PAPER 3

### SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI

1.
  - a) Taja mifano minane ya vipera vya utanzu wa semi katika fasihi simulizi. (alama4)
  - b) Fafanua sifa zozote tatu za mawaidha katika fasihi simulizi (alama3)
  - c) Eleza umuhimu tatu wa ngomezi. (alama3)
  - d) Eleza istilahi hizi za fasihi simulizi. (alama3)
    - i) Maghani
    - ii) Mapisi
    - iii) Misimu/simo
  - e) Fafanua sifa zozote tatu ambazo mtambaji wa hadithi anastahili kuwa nazo. (alama3)
  - f) Taja methali zozote mbili zilizo na dhana ya tashibihi. (alama2)
  - g) Eleza sifa zozote mbili za nyimbo. (alama2)

### SEHEMU YA B: USHAIRI

#### 2. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata

Mkata ni mkatika,harithi hatoridhiwa  
Sina ninalolishika,wala ninalochukuwa  
Mlimwengu kanipoka, hata tone la muruwa!  
Mrithi nini wanangu?

Sina ngo'mbe sina mbuzi,sina konde sina buwa  
Sina hata makaazi,mupasayo kuyajuwa  
Sina mazuri makuzi,jinsi nilivyoachwa  
Mrithi nini wanangu?

Sina kazi sina bazi ila wingi wa shakawa  
Sina chembe ya majazi mno ni kukamuliwa

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**

**E-mail:** [infosnkenya@gmail.com](mailto:infosnkenya@gmail.com) | ORDER ANSWERS ONLINE at [www.schoolsnetkenya.com](http://www.schoolsnetkenya.com)

Nakwa'cheni upagazi,ngumu kwenu ku'tuwa  
Mrithi nini wanangu?

Sina sikuachi jina,mkata hatasifiwa  
Hata nifanye la mana,mno mi kulaumiwa  
Poleni wangu sana,sana kwenu cha kutowa  
Mrithi nini wanangu?

Sina leo sina jana,sina kesho kutwaliwa  
Sina zizi sina shina,wala tawi kuchipuwa  
Sina wanangu mi sina,sana la kuacha kuraduwa  
Mrithi nini wanangu?

Sina utu sina haki,mila yangu meuliwa  
Nyuma yangu ili dhiki,na mbele imakaliwa  
N'na wana na milik,hadi nitakapofukiwa  
Mrithi nini wanangu?

Sina ila kesho kwenu,wenyewe kulongowa  
Muwane kwa nyinyi mbinu,mwende pasi kupumuwa  
Leo siyo kesho yenu,kama mutajikamuwa  
Mrithi nini wanangu?

### **MASWALI**

- a) Taja mambo yoyote mawili ambayo mtunzi angewarithisha wanawe. (alama2)
- b) Eleza sababu ya mtunzi kutoweza kuwarithisha wanawe. (alama3)
- c) Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alama4)
- d) Dondoa mifano miwili miwili ya:  
  - i. Inkisari
  - ii. Tabdila
- e) Chambua shairi hili kwa upande wa:

- i. Dhamira (alama2)
- ii. Muundo (alama4)
- f) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kama vilivyotumiwa katika shairi. (alama3)
  - i. Mlimwengu kanipoka
  - ii. Sina konde sina buwa.
  - iii. Wingi wa shakawa.

### **SEHEMU YA C: RIWAYA**

#### **A.K Matei: Chozi la Heri**

3. Malezi ya watoto katika riwaya ya Chozi la Heri ndicho kitovu cha ufanisi na matatizo yote yanayowapiku watoto. Jadili (alama 20)
4. "..., Di, ni mimi... niko hai. Auntie Sauna alishikwa na polisi. ”
- a) Liweke dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)
  - b) Fafanua sifa za msemaji. (alama 6)
  - c) Eleza tamathali moja ya lugha iliyotumika katika dondoo hii. (alama2)
  - d) Sauna alishikwa na polisi? Elezea kikamilifu (alama 8)

### **SEHEMU YA: D HADITHI FUPI**

#### **A.Chokocho na D.Kayanda:**

#### **Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyinginezo**

5. "Penzi lenu na nani? . . . Mgomba changaraweni haupandwi ukamea. Potelea mbali mkate wee!"
- a) Eleza muktadha wa dondoo hii. (alama 4)
  - b) Taja na ufafanue mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 4)
  - c) Onyesha vile maudhui ya utabaka yanavyojitokeza katika hadithi nzima. (alama 6)
  - d) Eleza sifa sita za mzugumzaji kwenye dondoo. (alama 6)
6. Kwa kurejelea hadithi zozote tano katika diwani ya, ‘Tumbo lisiloshiba na hadithi nyingine.’ Jadili maudhui ya nafasi ya wazazi katika malezi. (alama 20)

**SEHEMU YA E: TAMTHILIA**

**P.Kea: Kigogo**

7. Tamthilia ya “Kigogo” ni kioo cha uhalisia wa maisha ya jamii nyingi za Kiafrika. Thibitisha.